Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | July-2020|
Received: 27.06.2020; Accepted 30.06.2020; Published on 30.07.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

# Upambanuzi wa changamoto za vijana kama inavyodhihirika katika riwaya teule za Walibora

**Harrison Onyango Ogutu[1]; Prof. James Onyango Ogola [2]; Prof. Wendo Nabea[3]**

**[1,2,3] Idara ya Lugha, Fasihi na Isimu, Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya**

**Main Author Email: harrynamasumbi@gmail.com**

## IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kubaini changamoto zilizowakabili vijana katika mazingira walimoishi kwa mujibu wa riwaya za Walibora ambazo ni *Kufa Kuzikana, Ndoto ya Almasi na Kidagaa Kimemwozea.* Utafiti huu ulielekezwa na nadharia ya uhalisia ambayo hushughulikia uwasilishi wa uhalisi na ukweli wa mambo katika fasihi. Imani ya mhalisia ni kwamba kazi ya fasihi huwaweka wanajamii katika ulimwengu wao wa kawaida, kweli na halisi. Mihimili ya uhalisia iliotumika katika utafiti huu ilikuwa; nguzo ya kielelezo inayosisitiza uigaji wa hali halisi kwa njia ya kweli, wazi na sahihi; nguzo ya matumizi ya lugha ya wakati uliopo na inayosheheni uhalisi na ukweli wa mambo kama yalivyo katika jamii husika ilitumika. Njia kuu ya utafiti huu ilikuwa utaratibu wa upekuzi wa yaliyomo katika ukusanyaji data huku mbinu ya kithamano ikitumika kuchanganua na kueleza data ya visa na matukio yaliyodhihirisha changamoto dhidi ya vijana. Utafiti huu ulijikita katika muundo wa kimaelezi ambao ni sahili na kueleza mambo yanavyojitokeza kwa uyakinifu.Utafiti huu ulilenga wahusika vijana katika riwaya za Walibora huku akiangazia changamoto zilizowakabili. Mtafiti alitumia sampuli ya kimaksudi ambapo riwaya alizozifanyia utafiti aliziteua kwa kudhamiria kuwa zilisheheni maudhui mengi yaliyohusu changamoto halisi zilizowakabili vijana katika jamii yao. Data iliyokusanywa ilijumuisha maudhui yenye changamoto halisi zilizowakabili vijana kama vile ufisadi, ubaguzi, umaskini na ukabila. Utafiti huu ulinuiwa kuwa na natija kwa wasomi, wahakiki na watafiti wa masuala ya lugha na fasihi kwa kuwa sehemu ya kurejelewa na pia kuhamasisha jamii kuhusu changamoto za vijana ili kusaidia kutafuta suluhu kwa changamoto hizo.

**Maneno Muhimu:** Changamoto za vijana, kijana

**How to cite this article in APA (6th Edition)**

Ogutu, H. O., Ogola, O. &. Nabea, W. (2020). Upambanuzi wa changamoto za vijana kama inavyodhihirika katika riwaya teule za Walibora. *Editon Cons. J. Kiswahili,* 2(1), 89-97.

---------------------------------------------------------------***---------------------------------------------------------------



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | July-2020|
Received: 27.06.2020; Accepted 30.06.2020; Published on 30.07.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili*., Double –Blind Peer Reviewed Journal

## Utangulizi

Kwanza, watafiti, wahakiki pamoja na wasomi wengine wa maswala yanayohusu vijana katika fasihi watakuwa na msingi mzuri wa kurejelea wanapofanya kazi zao. Kwa njia moja au nyingine, matokeo ya utafiti huu yalinuiwa kuwafaa wasomi, wahakiki, watafiti na wataalamu wengine wa fasihi na lugha katika kazi zao hasa zile kazi ambazo zitajikita katika mambo yanayohusu vijana katika fasihi. Kutokana na mapendekezo ya utafiti huu, watafiti na wasomi wengine wataweza kuibuka na mada zingine nyingi za utafiti kwa nia ya kuisaidia jamii. Vijana hukumbwa na kukabiliwa na changamoto nyingi zinazotinga juhudi zao za kuafikia matamanio yao. Ni kutokana na hali hii mbovu ya vijana ulimwenguni ambapo kumekuwepo na utetezi wa hali ya vijana kote ulimwenguni.

Utafiti huu hivyo basi, ulijikita katika utanzu wa riwaya, hususan zile zilizoandikwa na mwandishi Ken Walibora. Riwaya zilizoteuliwa na mtafiti zilikuwa *Kufa Kuzikana, Ndoto ya Almasi na Kidagaa Kimemwozea.* Ingawa wahakiki kadhaa walishughulikia riwaya za Walibora huku wakiangazia vipengele mbalimbali vya fani, suala la changamoto zilizowakabili vijana ama kwa hakika halikushughulikiwa. Hivyo basi, ni kwa misingi hiyo ambapo mtafiti alichunguza riwaya teule; *Kufa Kuzikana, Ndoto ya Almasi* na *Kidagaa Kimemwozea* ili kujaza pengo hilo.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Ngara (1982) akichanganua riwaya ya *Arrow of God (1974)* ya Chinua Achebe, alibaini matatizo na migongano mbalimbali kwa mfano mgongano wa utamaduni na mila unaodhihirishwa na mhusika Umuoro ambaye aliishi kwa kuzingatia utamaduni hata ingawaje sehemu nyingi za nchi ya Nigeria zilikuwa zimeathiriwa sana na utamaduni wa kigeni.Ingawaje Ngara aliliangazia suala la utamaduni kama chanzo cha migongano katika jamii, hakuweza kuonyesha iwapo utamaduni huo ulikuwa changamoto kwa wahusika vijana na vile vile madhara ya utamaduni huo yalikuwa yapi. Kwa misingi hiyo basi, mtafitialitaka kubaini iwapo utamaduni na mila ulikuwa tatizo kwa vijana

Ongeti (1997) anakubaliana na Syambo kuwa vijana wamepevuka kielimu na kimawazo. Katika tamthilia ya *Visiki,* Ongeti anasema kuwa vijana huamka mapema kwenda kufanya kazi shambani na wazazi wao. Hata hivyo, Ongeti hakudhihirisha ukweli kuwa huku kuamka asubuhi kwa vijana kwenda shambani na wazazi wao wakati wanafaa kuwa shuleni ni changamoto kwa maisha ya vijana. Ni kwa misingi hii basi utafiti huu ulinuia kuangazia changamoto zinazowakabili vijana katika sekta mbalimbali za kijamii ikiwemo elimu.

Tahakiki ya *Mke Mwenza* iliyofanywa na King'ala (1986) ilionyesha matajiri wakitumia pesa zao kuwadhulumu watoto na vijana kimapenzi. Ingawaje King'ala alionyesha namna matajiri walivyotumia hela kuwadhulumu vijana kimapenzi, alikosa kutaja iwapo tendo hili ni changamoto sugu lililowakumba vijana. Ni kutokana na pengo hili ambapo mtafiti alilenga kudhihirisha kuwa vijana walikabiliwa na changamoto ayami zikiwemo dhuluma za kimapenzi zilizotekelezwa na watu wenye nafasi katika jamii.

Watoto wakiwemo vijana hunyanyaswa kimapenzi. Hii ni kwa mujibu wa Nganje (1993) akihakiki tamthilia ya *Masaibu ya Ndugu Jero.* Alidai kuwa mhusika yeyote msichana aking"ara huvutia ndugu Jero. Bila shaka hii ni dhuluma dhidi ya vijana wasichana. Ingawaje swala la mapenzi kati ya watu wazima na vijana liliangaziwa na huyu mtaalamu, hali hii haikuchukuliwa kama changamoto dhidi ya vijana. Hivyo basi, mtafiti alilenga kujaza pengo hili kwa kubaini changamoto dhidi ya



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | July-2020|
Received: 27.06.2020; Accepted 30.06.2020; Published on 30.07.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

vijana kama ilivyodhihirika katika riwaya teule za Walibora.

Topan (1975) na Mlacha (1985) walichambua tamthilia ya Hussein (1971), *Wakati Ukuta.* Katika uchambuzi wao walilenga maudhui ya mgongano wa utamaduni baina ya wanaong'ang'ania usasa na upande mwingine wanaong‟ang‟ania ukale. Wawili hawa walithibitisha kuwa Hussein (1971) alifaulu kuonyesha kuwa utamaduni wa kizungu ulichangia utovu wa tabia miongoni mwa vijana waliopata elimu ya kizungu. Topan na Mcha hata hivyo hawakubainisha iwapo utamaduni wa kiafrika na kizungu uligongana kiasi cha kuwa changamoto dhidi ya vijana chipukizi. Kuambatana na ukweli huu basi, mtafiti alilenga kubaini iwapo migongano ya utamaduni huwatatiza vijana.

Mugambi (1982) alihakiki maudhui katika tamthilia za Kiswahili za Kikenya zilizochapishwa baina ya miaka 1956-1982. Katika uhakiki huo alitumia nadharia ya Ki-marx. Mojawapo ya tamthilia alizozishughulikia ni *Uasi*. Katika tamthilia hiyo, Mugambi alionyesha maudhui ya Uasi ambao ulitekelezwa na vijana dhidi ya wazee na mila za jamii yao. Hata hivyo, Mugambi alihoji kuwa vijana waliopinga mila tayari walikuwa wameathiriwa na ubabe dume kwani wao waliwaona wanawake kama vyombo. Tofauti na kazi ya Mugambi, mtafiti alinuia kuangazia changamoto zilizowakabili. Kwa hivyo, utafiti huu ulilenga kubaini iwapo mila zilizoshikiliwa na wazee ni changamoto dhidi ya vijana katika jitihada zao za kutaka kuboresha maisha.

Vijana katika tamthilia ya *Uasi* waliasi dhidi ya mila zilizopitwa na wakati kama vile wazee kuwaoa wasichana „wabichi‟wanaopaswa kuwa mabinti zao. Mgogoro huu wa wahusika vijana dhidi ya wazee ulishughulikiwa na Wafula (1999) katika uchambuzi wake wa *Uasi.* Vijana hivyo basi walikabiliana na mila na tamaduni ambazo kulingana nao hazifai kuzingatiwa katika ulimwengu wa kisasa. Mila hizi pamoja na tamaduni zilikuwa changamoto kwa maisha ya vijana. Kibet (2005) alichanganua namna Burhani anavyotatua matatizo yanayowakabili wanajamii katika riwaya zake akitumia nadharia ya mgongano iliyo na asili yake katika Umarx kama ilivyofafanunuliwa na wanasoshiolojia. Rotich alishughulikia matatizo mbalimbali yanayokabili jamii kwa jumla na namna ambavyo matatizo hayo yangeweza kutatuliwa kwa mujibu wa mtunzi. Utafiti wa Rotich unatofautiana na utafiti huu kwa misingi kuwa utafiti huu unajishughulisha na changamoto zinazowakumba vijana katika kazi za Walibora. Vile vile utafiti huu ulitumia nadharia ya uhalisia bali sio Umaksi.

Msokile (1993) alijadili umuhimu wa kilele katika kazi ya fasihi. Kulingana naye kilele kinafaa kukidhi kiu au haja ya msomaji. Haja ya msomaji yaweza kuwa ni kuona changamoto mbalimbali.Utafiti huu hivyo basi, ulifaa kwa sababu ulichunguza changamoto zilizowakabili vijana katika riwaya za Walibora. Msokile (1993) vile vile alijadili dhima na wajibu wa mhakiki. Kulingana naye mhakiki ana wajibu wa kuamua ubora wa kazi ya sanaa. Tofauti na mawazo ya Msokile, utafiti huu ulitathmini namna Walibora alivyofaulu kuibua na kuangazia changamoto zilizowakabili vijana kwa njia sahihi, kweli na halisi.

Senkoro (1982) alizungumzia maudhui katika kazi ya fasihi na tahakiki. Hata hivyo izingatiwe kuwa katika kazi yake, Senkoro alijishughulisha na suala la migongano na umuhimu wake katika kukamilisha kazi ya kisanii ilhali utafiti huu nao ulichunguza suala la changamoto dhidi ya wahusika vijana kama alivyodhihirisha Walibora katika riwaya zake teule.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | July-2020|
Received: 27.06.2020; Accepted 30.06.2020; Published on 30.07.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

Njogu (1997) anaonyesha katika riwaya za *Visiwani Zanzibar* kuwa kulikuwa na mivutano mikubwa ya kitabaka baina ya walio navyo na wasiokuwa navyo. Katika tahakiki yake amebainisha namna mikinzano ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ilivyochochea mapinduzi. Njogu alijadili namna mikinzano ya kitabaka ilivyochochea mapinduzi ya kijamii katika riwaya kama vile *Asali Chungu (1980), Dunia Mti Mkavu (1980), Utengano (1980), Kiu (1972), Nyota ya Rehema (1976)* na zingine. Utafiti wa Njogu unatofautiana na huu wetu kwa misingi kuwa Njogu hakuangazia mikinzano hiyo ya kitabaka kama changamoto dhidi ya vijana. Matatizo ya migongano katika riwaya ya *Walenisi (1995)* ya Katama Mkangi yalichunguzwa. Wamitila (2003) aliangazia matatizo kama vile ujinga, magonjwa na dhuluma. Aliendelea kusema kuwa hali hiyo ilitokana na ubaguzi wa aina mbalimbali ukiwemo dini, ukabila na rangi. Kwa mujibu wa Mkangi, matatizo hayo yaliathiri jamii na ulimwengu mzima. Kinyume na utafiti huo wa Wamitila, utafiti huu ulimulika changamoto zilizowakabili wahusika vijana bali sio jamii nzima.

Watafiti kama vile Kimani Njogu (1997) na Njogu na Chimerah (1999) walionyesha namna wanariwaya kama S.A Mohamed, M.S Mohamed, S.A Shafi na George Orwell walivyomulika na kutatua matatizo mbalimbali katika jamii. Watafiti hao walijadili na kuonyesha namna matatizo ya jamii yangesuluhishwa kwa kutumia mapinduzi. Waliangazia matatizo ya jamii kwa jumla kinyume na utafiti huu uliomulika changamoto zilizowakabili wahusika vijana katika jamii mujibu wa Walibora katika riwaya zake teule.

**MUKHTASARI**

**Changamoto Zinazowakumba Vijana: Mifano Kutoka Riwaya Za Walibora**

**Umaskini**

Katika uchanganuzi wake, mtafiti aligundua kuwa vijana wengi katika riwaya teule waliishi katika umaskini. Kwanza kabisa, mhusika Amani, kijana wa umri wa miaka ishirini na minne (24) katika *Kidagaa Kimemwozea*, yasemekana alikuwa kijana maskini mwandishi anaposema; "Pembeni, alikuwa na mkoba mdogo mweusi uliobeba kila kilichokuwa chake. Alikuwa kavaa shati la nili lililodondosha vifungo. Suruali yake ya kaki ina viraka viwili vikubwa vya urujuani vilivyochungulia makalioni kama pazia kwenye madirisha ya nyumba", (uk 1). Taswira aliyoipata mtafiti kutokana na maelezo hayo, ni wazi kuwa kijana Amani aliishi maisha ya ukata. Kwanza, mali yake yote ilibebwa katika mkoba mdogo mweusi, pili shati lake lilikuwa limedondosha vifungo na tatu suruali yake ya kaki ilikuwa na viraka vikubwa vya urujuani vilivyochungulia makalioni kama pazia kwenye madirisha ya nyumba.

**Udhalimu**

Katika riwaya lengwa dhuluma ilijitokeza dhahiri shahiri katika asasi mbalimbali za kijamii zikiwemo sekta za afya (matibabu), taasisi za elimu (shule na vyuo) na hata utamaduni na desturi za jamii. Katika *Ndoto Ya Almasi*, utepetevu na mapuuza ya daktari yalimfanya kijana Almasi kufungwa jela ya watu wakomavu. Daktari alitoa ripoti ya umri wa Almasi kwa kumwangalia tu kwa macho. Daktari alipuuzilia mbali ukweli wa Almasi kuhusu umri wake kamili. Mwandishi anasema, "Almasi alipofikishwa hospitalini na askari polisi, daktari alimkagua kwa macho makali na kumwuliza, una umri gani?" Akajibu, "kumi na saba." Kisha daktari akaandika ripoti yake na kuibana kwenye bahasha… hakimu alipoisoma ripoti hiyo na kusema daktari kaandika ati umri wa miaka 19" (uk 12). Ni dhahiri kuwa daktari hakumtendea kijana Almasi haki. Tendo la kumwongezea miaka mingine miwili



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | July-2020|
Received: 27.06.2020; Accepted 30.06.2020; Published on 30.07.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

lilimfanya Almasi afungwe katika jela ya watu wazima kinyume na sheria ambayo hairuhusu mtu asiyefikisha miaka kumi na minane kufungwa jela ya watu wazima. Tendo hilo la daktari kwa kijana Almasi ni dhuluma.

**Mapenzi kabla ya Ndoa na Ndoa za Mapema**

Raha, anasa na mapenzi kabla ya ndoa ni mojawapo ya changamoto kubwa zilizowakumba vijana katika riwaya lengwa. Kijana msichana Lowela katika *Kidagaa Kimemwozea*, alijiingiza katika raha na anasa akaathirika kiasi cha kuacha masomo yake. Inasemekana kuwa; "Lowela alikuwa kaachia shule kwenye kidato cha tatu ili atumbue maisha maana kufa kwaja. Ni kama ndege arukaye juu kwa juu na kutua popote atakapo muradi mbawa zingalipo. Na maadamu alikuwa hai lake kubwa kuhanjahanja, wa kufyotoka hakuna" (uk11). Katika uchanganuzi wake, mtafiti alibaini kuwa kijana Lowela alishindwa kudhibiti hisia za mwili ikabidi aachie shule Kidato cha Tatu ili aponde raha kufa kwaja. Aliishi kuhanjahanja huku na huku bila kujali. Huku kukosa kujidhibiti na mwishowe kujiwachilia katika raha, anasa na mapenzi kabla ya ndoa ni changamoto dhidi ya kijana Lowela.

**Kutowajibika**

Kuna visa vingi katika riwaya lengwa ambavyo vinadhihirisha mapuuza dhidi ya vijana kama changamoto kuu. Kwa mujibu wa *Kidagaa Kimemwozea,* kijana msichana Mashaka, alikosa kuwajibikia maisha yake ya baadaye alipojihusisha katika usuhuba na mapenzi na kijana Ben Bella, mvutaji bangi na sugu wa jela. Mashaka alisitisha masomo yake Ben Bella alipovunja uhusiano wao. Mashaka alisononeka na kuwehuka kiasi cha kutembea uchi. Hii ni hali ambayo Mashaka angeepuka iwapo hangejihusisha katika usuhuba kabla ya ndoa. Kutowajibika kwake kulimwingiza katika hali hii ya wehu.

**Uraibu wa Vileo na Mihadarati**

Matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, pombe na sigara ni changamoto kubwa kwa vijana. Almasi katika *Ndoto ya Almasi,* alijifunza kuvuta sigara akiwa katika jela. Uvutaji wa sigara, mtafiti aligundua kuwa ilikuwa tabia ya ufungwa. Uraibu wa sigara ulikuwa changamoto kubwa kwa kijana Almasi. Alitamani kuacha lakini ukawa umemfunga kwa mikatale ya utumwa wa milele. Mara nyingi kijana Almasi alikuwa amekiri kuacha kuvuta sigara. Lakini yaonekana alishindwa kabisa kuacha tabia hii. Mwandishi anasema, "…akamkuta Almasi amekalia kitanda ananyonya na kuifyonza ibilisi iitwayo sigara huku macho ameyatoa pima kwa uraibu uliomfunga mikatale ya utumwa wa milele", (uk 60-61). Tabia ya uvutaji sigara ilimbadilisha Almasi akawa anatoa harufu mbaya – harufu ambayo ilisababisha akataliwe na mpwa wake, Dina. Tabia hii pia ilimuudhi mamake Almasi ingawaje alimkubali kama mtoto wake pengine kutokana na kuzoea tabia hiyo kutoka kwa mumewe mzee Masasi au kutimiza msemo usemao, uchungu wa mwana ajuaye mama.

**Vifo vya Wazazi**

Kijana Amani katika *Kidagaa Kimemwozea* uk 33, alifiwa na babake na mamake. Mamake alikufa ajali barabarani Amani akiwa na umri wa miaka ishirini. Maskini baba mtu kajifia kwa maradhi kabla ya mauaji ya babu yake. Kutokana na vifo vya wazazi wake, hasa mamake aliyekufa mwisho, Amani alizidiwa na jakamoyo, huzuni na usonono.

**Hali Mbaya ya Kiuchumi na Ajira Duni**

Amani, Imani na Bob DJ ni vijana wadogo ambao waliangukia ajira duni. Mwandishi anasema kuwa Imani na Amani walikuwa baadhi ya wachochole walioangukia kazi zisizotamanika. Kazi hizo zilikuwa



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | July-2020|
Received: 27.06.2020; Accepted 30.06.2020; Published on 30.07.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili*., Double –Blind Peer Reviewed Journal

utopasi, ufagizi, ulezi, utwana, ujakazi, umanamba na nyingine za sampuli hiyo. Amani alipata kazi ya uchungaji wa ng"ombe kwa mtemi Nasaba Bora kwa mshahara mdogo wa kijungujiko. Imani alipata ujakazi kwa mwalimu Majisifu kwa mshahara duni vile vile. Kazi ya Imani ilikuwa kupika chakula, kufua nguo nyingi sana, kupiga nyumba deki na kadhalika. Mwandishi akithibitisha hali hii katika *Kidagaa Kimemwozea* anasema, "Imani na Amani walikuwa baadhi ya wachochole walioangukia kazi zisizotamanika kama vile utopasi, ufagizi, ulezi, utwana, ujakazi, umanamnba na zingine za sampuli hiyo….Wote walipaswa kugeresha kuwa mishahara yao duni ilitosha. Yaani hali zao mbaya lakini si mbaya kama halaiki ya wasiokuwa na ajira ya aina yoyote" (uk 25).

**Ufisadi,Ukabila na Upendeleo wa undugu**

Kulingana na mtafiti, mwandishi wa riwaya teule alionyesha swala la ukabila,ufisadi na upendeleo wa undugu kuwa changamoto kubwa inayowakabili vijana katika jamii.Vijana walilazimika kutoa hongo au mlungura katika afisi za umma ili kupata huduma muhimu. Vile vile vijana walishuhudia watu wengi (raia) wakishikwa na polisi ili watoe hongo, *Kufa Kuzikana,* uk 16. Wale hawakuweza kutoa hongo walilazimika kulala korokoroni. Kulingana na kijana Tim, askari polisi waliwashika watu ovyo ovyo bila sababu yoyote na kuwahangaisha kana kwamba wakaua. Wale walikataa kutoa hongo walifunguliwa kesi mahakamani na kuwekewa makosa. Huo ni ufisadi wa kiwango cha juu na changamoto kwa vijana waliopatikana katika hali kama hii.

**Usaliti**

Katika utafiti huu, mtafiti alimulika usaliti kama changamoto dhidi ya vijana hasa usaliti unaotekelezwa na viongozi. Kuna baadhi ya vijana ambao walisalitiwa na viongozi wao ambao wangefaa kuwawajibikia. Mathalani, Mtemi Nasaba Bora katika *Kidagaa Kimemwozea* alimsaliti kijana msichana Lowela kwa kushiriki naye uasherati na hata kumtunga mimba jambo ambalo lilimfanya Lowela kuacha masomo akiwa Kidato cha Tatu ili aponde raha. Kwa hakika, Lowela alistahili kuwa bintiye, lakini kwa kiongozi huyu aliyefaa kusisitiza umuhimu wa masomo hasa kwa vijana wasichana kama Lowela, kushiriki naye katika uasherati na kumtunga mimba, ni usaliti mkubwa.

**Mila na utamaduni**

Mtafiti katika kazi hii aligundua kuwa baadhi ya mila na tamaduni katika jamii huzamisha ndoto za vijana Jamii ya Wabukusu ambamo kijana Almasi alizaliwa ni jamii ambayo ilieenzi tohara ya wanaume kama mboni ya jicho na kupokezana kama hirisi ya kinga. Kwa njia hiyo hiyo, jamii ya Wakalenjin ambayo ilionekana kutangamana sana na Wabukusu pia ilienzi sana tohara ya wanaume sawa na wanawake. Tohara ya lazima katika jamii iliwatia vijana hofu hasa kutokana na athari zake. Mwandishi wa *Ndoto ya Almasi* alithibitisha hayo, "Wazo la ngariba na tohara lilimtetemesha (Almasi) kiasi. Maskini kafungwa jela kabla ya kukutana na kisu cha ngariba", (uk 12). Kijana Almasi alifahamu fika kuwa vijana wengi waliishia kwenda hospitali kutibiwa majeraha yaliyotokana na kisu cha ngariba. Baadhi ya vijana hata walipoteza maisha yao baada ya kuvuja damu kupindukia kutokana na athari za kisu cha ngariba. Wazo la kisu cha ngariba hivyo basi lilimtia Almasi kiwewe.

**Kukataliwa**

Katika uchunguzi uliofanywa na mtafiti, ilibainika wazi kuwa baadhi ya vijana katika riwaya lengwa walikataliwa kwa misingi ya viwango vilivyowekwa na utamaduni na mila za jamii husika.. Mfano mzuri wa kijana aliyekabiliana na changamoto ya kukataliwa ni Almasi na dadake Nakhumicha. Mathalani, Almasi



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | July-2020|
Received: 27.06.2020; Accepted 30.06.2020; Published on 30.07.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

aliposingiziwa na kudhaniwa kuhusika katika mgomo shuleni uliosababisha kifo cha mwalimu mkuu Bwana Kipsang na hatimaye kufungwa jela kwa miaka minne, babake, Mzee Masasi alimkataa. Kwa mujibu wa *Ndoto ya Almasi,*uk 19, ni mamake Almasi tu ambaye angedhubutu kumtembelea katika jela huko Eldoret. Almasi alisema kwamba alisingiziwa kwa tuhuma za uongo akafungwa jela. Ni dhahiri kuwa wale waliomsingizia hawakumtakia mema, yaani walimkataa Almasi kutokana na tabia yake ya kutojihusisha na wenzake katika migomo na mipango miovu. Vile vile baba mtu hakuwahi mtembelea akiwa jela, kumaanisha kakutaka kujihusisha na mwanake aliyedaiwa kuwa mhalifu.

**Shinikizo la Wanarika na Utovu wa Nidhamu.**

Mtafiti alibaini kuwa utovu wa nidhamu ulikuwa umeenea sana katika taasisi za masomo. Mathalani, katika utafiti huu, mhusika Almasi alipojiunga na shule ya upili ya St. Joseph, alilakiwa kwabughudha, kero na dhuluma isiyomithilika. Almasi alipewa kiatu kilichonuka, akaamrishwa ampigie mamake simu. Alitemewa mate, akatukanwa, akamwagiwa maji baridi kitandani na kulazimishwa kufua nguo na kupiga viatu rangi. Wanafunzi waliwanyanyasa wenzao kwa kuwatusi na hata kuwaibia chochote walichokuwa nacho hata pesa. Utovu wa nidhamu miongoni mwa vijana vile vile ulikuwa wazi vijana wavulana walipowadhulumu vijana wasichana kingono. Vijana walisahau kilichowapeleka shuleni, wakajiingiza katika vitendo vya kihayawani. Mwandishi akieleza visa vya utovu wa nidhamu shuleni dhidi ya kijana Almasi katika *Kidagaa Kimemwozea.*

**Upotovu wa wanadini**

Katika riwaya lengwa, mtafiti aligundua kuwa uzandiki wa viongozi wa dini ulikuwa changamoto kubwa kwa wahusika vijana. Viongozi wa dini kama vile Kasisi John Njalala alikosa kuwa kielelezo kizuri kwa maisha ya vijana kama vile Tim, Pam, Akida na Jerumani.

Mtafiti akichanganua riwaya ya *Kufa Kuzikana*, alipata kuwa vita vya kikabila vilivyozuka Baraki, wilaya ya Korosho, nchini Kiwachema, vilichochewa na makasisi. Kwa mujibu wa habari alizokuwa nazo kijana Jerumani kutoka kwa jarida moja, nyumba za makasisi ndizo zilizokuwa mabohari ya bunduki, nyuta na mishale ya kuwamaliza watu wa Korosho. Kijana Akida alifikiria na kuamini kuwa pengine dini ingetumika kugeuza mioyo ya watu dhidi ya uovu kama vile ukabila. Lakini mtazamo wa Jerumani ulikuwa tofauti alipotoa kauli na madai yafuatayo;

> Dini? Wewe unaishi dunia gani Herr Madodo Kipande? Hujasikia Wakorosho walivyowauwa waumini wenzao Wakanju waliokimbilia usalama makanisani huko Korosho? Hujasikia nyumba za makasisi ndizo zilizokuwa mabohari ya bunduki, nyuta na mishale ya kuwamaliza watu wa Korosho. Mambo yale yale yaliyokuwa Rwanda ya wanadini kusahau dini na kuwaua wanadini wenzao kwa sababu za kikabila. Hujasikia mizozo na migawanyiko makanisani, mahekaluni na misikitini? (uk 156).

**Ubaguzi**

Vijana katika riwaya lengwa walibaguliwa kwa misingi ya mapendeleo ya kinasaba na pia ubaguzi wa rangi. Mathalani, kijana Jerumani alipoenda kusoma Ujerumani alikumbana na ubaguzi wa rangi. Alishiriki katika vita dhidi ya wazungu akimtetea mwanamke mwafrika mweusi kama yeye aliyekuwa akishambuliwa na hao wazungu. Wazungu wakamgeukia na kumjeruhi vibaya na hatimaye akapelekwa mahakamani alikofungwa miaka saba gerezani. Mwishowe



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | July-2020|
Received: 27.06.2020; Accepted 30.06.2020; Published on 30.07.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

alinyang"anywa ufadhili aliokuwa amepewa na serikali ya Ujerumani na hatimaye akaamrishwa kurudi nyumbani kwao Kiwachema. Jerumani anatupa kadhia hio katika *Kufa Kuzikana*; Wajerumani wameendelea kweli lakini wanamchukia mtu mweusi. Mtu anaonewa tu kwa sababu ya rangi ya ngozi yake ushafahamu? ....Nikawaona *skin heads* wane wanamshambulia mwanamke mweusi burebure akiwa na kitoto chake kidogo nje ya *Café Charmante* … Nikawarushia ngumi nzitonzito...walinitwanga nikaona vimulimuli…, (uk 155).

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO Hitimisho**

Uchanganuzi uliofanywa ulidhihirisha kuwa wahusika vijana katika riwaya teule walikabiliana na changamoto mbalimbali kwa mujibu ya madhumuni ya kwanza. Baadhi ya changamoto hizo ni kama vile umaskini, ukabila, ufisadi, matumizi ya madawa ya kulevya, udhalimu, mapuuza, vifo vya wazazi na unafiki wa wanadini.

**Mapendekezo**

Mtafiti anapendekeza waandishi wa kazi za fasihi waandike kazi zao wakianagazia manufaa ya kazi hizo kwa wanajamii hasa vijana ambao aghalabu hurejelewa kuwa viongozi wa kesho. Mtafiti anapendekeza kazi za fasihi zikiwemo riwaya zimulike uhalisia wa hali ilivyo katika jamii huku zikishughulikia changamoto za kila siku zinazowakumba wanajamii na kupendekeza njia mwafaka za kutatua changamoto hizo. Vile vile ni muhimu wahusika vijana wasawiriwe wakiwa katika mazingira ya uongozi ili kuwapa vijana matumaini ya kuongoza. Viongozi vijana waonyeshwa wakitatua matatizo na kukabiliana na changamoto mbalimbali kwa ufanifu mkubwa. Kwa njia hiyo, vijana katika jamii wanaweza kuwa na kielelezo katika harakati za kukabiliana na changamoto hizo.

**MAREJELEO YA KIMSINGI**

Walibora, K (2003). *Kufa Kuzikana.* Longhorn Kenya Ltd; Barabara ya Funzi, Eneo la Viwandani, Nairobi, Kenya.

Walibora, K. (2006). *Ndoto ya Almasi.* Moran (E.A) Publishers Limited, Judda Comlex, Forest Road, Nairobi, Kenya.

Walibora, K. (2012). *Kidagaa Kimemwozea.*Target Publications Limited, Jengo la Devan, Barabara ya Chiromo, Eneo la Westlands, Nairobi, Kenya.

**MAREJELEO MENGINE**

Hussein, E. N. (1971). *Wakati Ukuta.* Nairobi: East African Publishing House. Kenyatta Foundation.

Kibet, R . P. (2005) "Uchanganuzi wa namna Burhan anavyotatua matatizo yanayokabili jamii katika riwaya zake". Egerton. Tasnifu ya M.A

King'ala. Y. M. . (1986). *Mbinu za Fasihi: Uchambuzi wa Riwaya na Tamthilia.*KenyaLiterature Bureau. Nairobi Ltd, London.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | July-2020|
Received: 27.06.2020; Accepted 30.06.2020; Published on 30.07.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Mlacha (1985) "Wahusika katika Riwaya za Kiswahili" Tanzania 1970-1982 mulika 17. Jarida la TUKI. Chuo Kikuu cha Dar es salaam.
Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* East African Educational Publishers Ltd.
Mugambi, P. J. M. (1982). *Uhakiki wa Maudhui katika Tamthilia za Kiswahili za kikenya zilizochapishwa*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa). Nairobi.
Nganje, D. K. (1993). *Mwongozo wa Masaibu ya NduguJero*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
Ngara, E. (1982) *Stylistic Criticism and the African Novel.* Heinemann Educationa Books
Njogu, K. (1997) *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar.* Kenya. Nairobi University Press.
Njogu, K., &Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.
Ongeti, K. I. (1984). *Visiki.* East African Educational Publishers Ltd, Nairobi.
Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi.* Dar es salaam. Press and Publicity Center.
Topan, F . M. (1975). Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili. Dar es salaam. Oxford
Topan. F. M (1977). Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili. Dar es salaam. Oxford University Press.
Universty Press.
Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo Yake.*Nairobi; Jomo
Wamitila, K. (2003). *Kichocheo cha Fasihi.*Nairobi, Focus publications Ltd.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org